TANGAZO LA SERIKALI NA. 223 la tarehe 22/3/2019

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1)(z) na 16 (1).*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA, 2019

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, za Mwaka 2019.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo-

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya;

"hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada, katika mwaka wa mapato;

"jumuisho" maana yake ni taarifa, nyaraka au hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizo zalishwa, zilizo sambazwa, zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara na ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au

la mwisho;

"kipindi cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mkusanya ushuru" maana yake ni mtumishi wa Halmashauri au Wakala aliyeteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria Ndogo hizi;

"mwaka wa mapato" maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka;

"taasisi ya kibiashara" maana yake taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya Makampuni au Sheria ya Majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa au mazao ya kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya Nchi;

"wakala" maana yake kampuni, au taasisi yoyote iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya au kufanya tathmini ya ushuru kwa niaba ya Halmashauri;

Ushuru wa Huduma

4. Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa Huduma kwa kampuni, taasisi ya biashara au tawi la kampuni au Mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) kutokana na uzalishaji wa bidhaa, kazi na huduma zinazofanyika ndani ya eneo la Halmashauri.

Wajibu wa kulipa Ushuru

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara, kampuni, taasisi ya biashara au tawi la kampuni kulipa Ushuru wa Huduma utokanao na utoaji wa huduma, kazi, mauzo ya bidhaa katika eneo la Halmashauri;

Taratibu za kulipa Ushuru wa Huduma

6.-(1) Kila Mfanyabiashara anayetakiwa kulipa Ushuru wa huduma , atawasilisha kwa Halmashauri taarifa za hesabu za mauzo kwa kila mwezi husika na atalipa Ushuru wa Huduma kwa mujibu wa viwango vitakavyotokana na ukokotoaji wa hesabu hizo au atalipa kwa mujibu wa Viwango vilivyotajwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi kwa wafanyabiashara wasio na vitabu vya hesabu;

(2) Endapo Mlipa Ushuru yeyote atashindwa kuwasilisha taarifa sahihi za mauzo kwa wakati, Mkurugenzi kwa maandishi anaweza kumtaka Mlipa ushuru huyo kuwasilisha taarifa hizo ndani ya siku thelathini zinazohusu kipindi maalum cha hesabu zikionyesha kiasi na thamani ya fedha za mauzo ya bidhaa zilizoingizwa, kusambazwa au kuuzwa, na kazi, au huduma zilizotolewa;

(3) Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa anaweza kumtaka kwa maandishi mtu yeyote mwenye taarifa kuhusu taasisi yoyote ya mfanyabiashara yoyote anayepaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa ambazo zitatumiwa kama taarifa sahihi.

Namna ya kulipa Ushuru

7.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa huduma utakaolipwa na makampuni, matawi ya makampuni, taasisi au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara katika eneo la mamlaka ya Halmashauri kwa kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu(0.3%) ya mapato halisi baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya mlaji.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (**1**) hapo juu, Mfanyabiashara ambaye hayuko kwenye kundi la wasiowasilisha hesabu zake Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) atalipa Ushuru wa Huduma kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Uwezo wa kufanya ukaguzi

8. Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia kwenye eneo lolote la Mlipa Ushuru kwa ajili ya kutafuta taarifa au kuchunguza hesabu, vitabu au taarifa zozote kama ataona inafaa na kufanya uchunguzi kwa jukumu la kulipa ushuru.

Makosa

9. Itakuwa ni kosa kwa Mtu yeyote endapo-

(a) atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi za biashara yake;

(b) atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Mkurugenzi au Afisa mwidhiniwa katika muda uliowekwa;

(c) atashindwa kutunza kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya ukokotoaji wa mahesabu ya kodi ya huduma;

(d) atafanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizosahihi;

(e) atatoa taarifa isiyo sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au jukumu la mtu mwingine linalohusu kulipa kodi ya huduma;

(f) ataandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya hesabu au kumbukumbu;

(g) atamzuia au atajaribu kumzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhinishwa au wakala kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(h) ataharibu kwa makusudi taarifa au mfumo wa taarifa

(i) ataharibu makusudi vitendea kazi vya kukusanyia kodi;

(j) atashidwa kwa namna yoyote kutekeleza Sheria Ndogo hizi;

Adhabu

10. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi Shilingi Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

11. Bila kuathiri kifungu cha 10 hapo juu, Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote anayedaiwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi ikiwa mdaiwa huyo amekiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kuahidi kuwa atalipa deni analodaiwa pamoja na faini ya isiyopungua shilingi laki mbili au isiyozidi shilingi Laki tano.

________

JEDWALI LA KWANZA

________

*(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 6(1))*

________

VIWANGO VYA USHURU KWA WAFANYABIASHARA WASIO NA VITABU VYA HESABU

| Na. | Aina ya biashara | Kiasi(Tshs) cha malipo kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1 | Maduka ya rejereja | 10,000/= |
| 2 | Maduka ya vifaa vya ujenzi | 20,000/= |
| 3 | Maduka ya jumla | 30,000/= |
| 4 | Maduka ya nusu jumla | 20,000/= |
| 5 | Maduka ya nguo | 20,000/= |
| 6 | Maduka ya Spea za magari | 25,000/= |
| 7 | Wauza bidhaa za kuchomelea | 10,000/= |
| 8 | Maduka ya bidhaa za umeme | 20,000/= |
| 9 | Maduka ya dawa | 10,000/= |
| 10 | Mashine za kusaga | 10,000/= |
| 11 | Karakana | 24,000/= |
| 12 | Maduka ya vipodozi | 16,000/= |
| 13 | Spea za Pikipiki | 10,000/= |
| 14 | Maduka ya vipodozi | 20,000/= |
| 15 | Biashara nyinginezo | 10,000/= |

________

JEDWALI LA PILI

________

*(Chini ya kifungu cha 11)*

________

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………… nakiri mbele ya ………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Mbeya kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma ) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya za Mwaka 2019.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, niko tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini iliyoelekezwa kwenye Kifungu 10 cha Sheria Ndogo hizi.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO YANGU YA HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KWA KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………..…. ya Mwezi…………………………… Mwaka ………………….
*Jina*……………………………………………….. *Saini*…………………………………….

Mbele ya :

Jina: ……………………………………………
Cheo: ………………………………………….
Saini: …………………………………………..

Lakiri na Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kilichofanyika tarehe 22 mwezi Agosti mwaka 2018 na ulibandikwa mbele ya:-

…………………………………..
STEPHEN E. KATEMBA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya*

**L.S**

……………………………………
MWALINGO MWAYONGO KISEMBA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya*

NAKUBALI,

Dodoma,
05 Machi, 2019

……………………………………….
SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*